Title: THE RESURRECTION
Preached by Dr. w euGENE SCOTT, PhD., Stanford University
At the Los Angeles University Cathedral
Copyright © 2007, Pastor Melissa Scott. - all rights reserved

SOMO: UFUFUO
Na Dk. W. euGENE SCOTT (Shahada ya Udaktari wa Salfasa, kutoka Chuo Kikuu Cha Stanford)
Imehubiriwa katika Kanisa Kuu la Chuo Kikuu Cha Los Angeles
Haki ©2007 - Mchungaji Melissa Scott – Haki zote zimehifadhiwa

# UFUFUO

Nilipoteza imani yangu nikiwa chuoni. Niliipoteza kwa sababu ya mgandamizo kidogo tu wa maisha. Ilikuwa rahisi sana kuamini kama Yesu ni "mwalimu mwema na mwerevu'', nilimlinganisha yeye sawa sawa mtume Mohammad, ambaye ni mwanzilishi wa imani ya Kiislam, pamoja na Gautama Buddha, ambae pia ni mwana wa mfalme wa India na mwanzilikishi wa imani ya Buddha, na "*Confucius*" wa China (na wana falsafa wengine wengi tu) ambao misemo yao kwa kifupi imekuwa na nguvu sana sehemu hizo za dunia, kama waanzilishi wengine maarufu wa dini.

Nilimuweka Yesu katika kundi hilo, nilimchukulia yeye kama "mwalimu mwema na mwerevu", aliyekubalika na kupata mbawa zangu za kitaaluma. Lakini kuamini kwamba Yesu Kristo alikuwa Mwana wa Mungu, hicho hakikuwa kitu rahisi kwangu. Kwa kifupi niseme kuna matangazo ya kwenye runininga na kaseti za mauzo zinazoelezea mwanzo wa dini zote.

Inaanzia Misri, lakini haiendi Sumer ambako dini zilianzia kisha kuelekea Misri (na hawakufika Babeli). Lakini hakuna awezaye kupinga ushawishi wa Misri kwa Waebrania na Wagiriki. Cyrus Gordon anakomea hapo.

Lakini katika hili tangazo kuna kijana mdogo aliyejengeka kimaumbile amekaa pale na Mwinjilisti mzuri anayejulikana kama Mwinjilisti wa kwenye Runinga anamtazama huyu kijana aliyekaa pale, wanakwambia jinsi dini zilivyoanza, na wakupa mfano mbadala wa watu 16 walionusurika katika kusurubiwa –ambao ni mfano kinyume na mazungumzo yao.

Mfano mwingine wa kisasa ni "Mtazamo wa dini wa pamoja" – Dini zisizo na Dini (kama ilivyoitwa na mmoja wa maprofesa wa Mlingano wa Dini katika Chuo Kikuu cha Stanford) kama wasemavyo, dini zote "zina mzizi mmoja." Mtazamo huo ulinijia, kwa ushawishi kwamba sitakuwa mwenye akili mpaka nifuzu " mtizamo huu wa kizamani" kumwangalia Kristo kama, ni mwana wa Mungu na mwenye uweza wa kiungu na kumkubali yeye kama mwanzilishi mwingine wa dini ambayo sio ya kawaida; ambayo ilipunguza tu makali ya mtazamo wa "mwalimu mwema na mwerevu."

Tazizo moja ni kwamba mbadala wa kitaalamu wa imani ndani ya uweza wa Mungu katika Kristo, unaojulikana kama "mwalimu mwema na mwerevu," aidha hawezi kuwa na sifa moja kati ya hizi bila lazima awe nazo zote yaani "mwalimu mwema na mwerevu".

Kuwa mwema, lazima uongee ukweli. Kwa hakika unaweza kuwa umepungukiwa na akili, unaweza kuwa hamnazo, kuamini uongo huu, kwamba mtu anaweza kuwa mwema lakini sio mwerevu. Kuwa mwerevu, lazima uwe sahihi; kuwa mwema, lazima uwe muwazi, na "Yesu wao" anaweza kuwa mwema lakini sio mwerevu, mwerevu lakini sio mwema, la hasha si vyote. Kwa nini?

Katika chanzo chochote ulichonacho kuhusu historia ya Yesu, kama ukimwita "mwema na mwerevu" lazima utakubaliana na maneno yake, na lazima utakubaliana na matendo yake. Sipingi vyanzo vya Injli, ingawa huko ndiko watu wengi wapinzani wa Kristo wanaenda wanapotafuta mistari ili kuelezea maisha ya Kristo and maneno yake na kuyaandika katika kwa msititizo kwa maadnishi mekundu kwenye Runinga.

Unaweza kwenda zaidi ya Injili. Kuna mfano "Q" wa nyaraka. Mmoja wa wazee wa kanisa wa mwanzo alisema kwamba Matayo aliandika maneno ya Kristo alipokuwa akisafiri naye, sio kwa Kigiriki, bali katika lugha yake ya asili ambayo inaitwa Aramaiki. Tunafahamu kwamba Injili yake yawezekana iliandikwa kule Antiokia na iliandikwa kwa Kigiriki. Haya "Maneno ya Yesu,"yaliyoandikwa Kiaramiki yaweza kuwa chanzo kikubwa cha Injili. Wenye kufahamu Kigiriki wanaweza kuona mabadiliko katika mtindo wa vifungu vya Injili, na wanaweza kuviunda upya hivi vifungu kupendekeza chanzo likichotumiwa na wandishi hawa watatu wa Injili, Mathayo, Marko, Luka (zaidi Mathayo na Luka).

Wasomi wengi wa kisasa wanamchukulia Marko kama ndiye aliyekuwa wa kwanza kuandika, kwa sababu tunaona mabadiliko ya mtindo wakati Mathayo na Luka wakimnakili Marko. Ushawishi mkubwa "katika chanzo vya Injili" katika vitabu vya kwanza vya Injili unaitwa mfano "Q" wa nyaraka (kwa Kijerumani "chanzo"). Unaweza hata kuangalia nyimbo za kale, nyimbo za mwanzo. Bado, unapokutana na Yesu anafanya au anasema kitu fulani, kinachoambatana au kuhusiana na hizo kumbukumbu kutakuwa na **msemo** **au** muiinuko wa **tabia/sifa** aliyonayo ambayo inazuia kumuita yeye "mwema **na** mwerevu" kwa sababu utakuta moja au hata zaidi ya yafuatayo katika kila chanzo:

1. **Alifikikri kuwa yeye ni mkamilifu.**

Haijalishi kama alikuwa, akifikiri alikuwa mkamilifu. Carlysle anasema kwamba dhambi kubwa kuliko zote ni kutotambua kitu chochote. Hakuna kitu cha aibu kuliko vyote kama mtu akifikiri kuwa hajawahi kufanya kosa. Huko kutojitambua, kujihesabia haki, ukamilifu sio vitu ambavyo tunaviitikia, kwa sababu hekima ya mwanadamu inajuimusha maarifa ambayo hakuna aliye kamili. Sasa tuangalie, jambo kubwa si kwamba Yesu alikuwa mkamilifu au la, hatuwaiti watu watakatifu ambao **wanafikiri** ni wakamilifu. Kumbukumbu ya watu waliotumiwa na Mungu waonajiona wenyewe kwamba si wakamilifu inapatikana katika Agano la kale lote – "Mimi sistahili hata kidogo hizo rehema zote – Mimi ni nani hata niwaongoze wana wa Israeli? – Lakini mimi ni mtoto. Siwezi kuongea."

Siku zote kipimo cha kukubaliwa na Mungu na kukubaliwa na mwanadamu ni kujitambua kwamba wewe si mkamilifu. Watakatifu wanaatambua umbali waliona na Mungu. Kuna mtu mmoja pekee aliyemuona Mungu; Katika mwaka ule aliokufa mfalme Uzia, Isaya ni mtu pekee aliyemuona

Mungu ameketi katika kiti cha enzi, kilicho juu sana na kimeinuliwa sana – hii ina maana kwamba alikuwa juu ya kila mtu. Ndipo aliposema: “Ole wangu mimi; Kwa maana nimepotea.”

Hatuwaiti watu kuwa ni watakatifu wanofikiri kuwa ni wakamilifu – lakini Yesu alifikiri alikuwa Mtakatifu. Kila sehemu unapokutana naye anajiinua hivyo. Anahukumu watu wengine: “makaburi yaliyopakwa chokaa;” “ nayo kwa nje yanaonekana kuwa mazuri, bali ndani yamejaa mifupa ya wafu.”Aliwangaliwa watu wenye haki wa siku hizo akawashusha chini. Sababu ni kwamba mtu yeyote hatakiwi kuhukumu, mtu yeyote nayehukumu lazima awe na dhamira hii, kwamba ni rahisi kuhukumu mwenzetu kwa sababu tunajua kiundani tuna udhaifu huo huo.

Lakini Yesu hakuwa na hata na chembe ya ukamilifu. Alibadilisha Sheria, akisema, “mmesikia ikisemwa kwenu kwamba, tazama nasema,” na tena, , mwenye haki na dhamira ya ukamilifu“, anasema, “msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la sikuja kutangua, bali kuitimiliza.”

Kuna mfano mmoja wa tofauti ukilinganisha na hiyo, wakati kijana tajiri alipoenda kwake na kusema, “Mwalimu Mwema.” Alimnyamazisha na kumwambia, “Kwa nini kuniita mwema?” Wale wanaotaka kumuongelea Yesu msifikiri kwamba alikuwa mkamilifu katika mstari huu; wakosa yote, kwa sababu Yesu alimwambia, “nisubiri dakika moja”. Usije na usiniite mimi mwalimu mwema. Kama ukiniita mimi mwema, pia lazima utambue kwamba Mungu pekee ndiye awezaye kuwa mwema, kwa hiyo, usitume huo msamiati bila kutambua kwamba mimi pia ni Mungu.”

Alikuwa na ukamilifu, na hakuna sehemu yoyote ambapo upungufu ulionekana ndani yake;

**2. Alikuwa na mamlaka yote**.

Alisema, nimepewa mamlaka yote: “ Jenga juu ya ninachosema, unajenga juu ya mwamba. Jenga kwenye kitu kingine chochote, jenga juu ya mchanga. Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.”

Tena kwenye maelezo mengine aliyoyatumia, alisema kuhusu Sheria (vizazi vya kukubaliwa vimewekwa juu yake): “Umesikia ikisemwa kwenu, lakini tazama nasema...” Aliitamka hukumu bila kukwepa.

Sasa, hatuwaiti watu wa aina hiyo watakatifu. Tuauliza sababu , “Unaangalia wapi kwenye huu mamlaka?” Alijiangalia mwenyewe: “Tazama, **nawaambia**...”

**3. Alijiweka mwenyewe katikati ya Dini za Ulimwenguni.**

Aliendelea zaidi na akajiiweka katikati ya dini za ulimwenguni. Yesu hakuhubiri mafundisho au kweli zaidi ya yeye mwenyewe. Alisema, “mimi ndimi njia. Mimi ndimi kweli. Mimi ndimi uzima. Pasipo mimi mtu hawezi kuingia... mimi ndimi mlango wa kondoo. Yeye asiye na baba, mama, mke, watoto, na maisha yake pia, ajitwike msalaba wake na anifuatue **nyuma yangu**, huwezi kuwa **Mfuasi wangu**.” Alifanya mahusiano na yeye, umeweke katitkati ya dini zote za ulimwenguni, kigezo cha manufaa yote ya kidini.

**4. Aliongelea Uzima wa Milele kwa kina**

Kuna mfano fulani halisi nyumbani kwako, kweli unaweza kusema, “Kochi la ofisi yangu ya nyumbani ni la rangi ya kahawia. Huwezi kuuliza, “umejuaje?” Tunaongelea mambo ya nyumbani “maarifa ya kina” na inakuja kwa jinsi hiyo. Wala hatubishi; tunategemea kuaminiwa. Huo ndio mfano wa kazi ya Yesu anapoongelea kuhusu uzima. Na kiukweli anasema, ‘’ninakwenda zangu’’. Ninakwenda kuwaandalia makao. Baada ya kitambo kidogo ‘’nitarudi nije niwachukue.”

Anasema tena: “Kabla ya Abramu, Nilikuwepo.” Au, tena, “Nimemuona Shetani akianguka chini.” Au, tena, “malaika mbinguni hushangilia mwenye dhambi anapotubu.” Alitufanya tuamini kwamba alikuwa na “maarifa ya kina” ya uzima kabla na baada ya kuumbwa kwa ulimwengu na “kwa kina” juu ya mbingu na Mungu.

**5. Alikufa na Kufanyika kuwa sadaka**

Alisema kitu fulani ambacho si kweli kwamba dunia yote itawekwa huru kwa yeye kufa, “sadaka” kwa hakika wasikilizaji wake walijua maana ya sadaka. Sadaka ilitolewa ili kurejesha urithi uliopotea, kuwakomboa walio katika hatma ya mauti kwa sababu ya makosa yao. Ilikuwa ni kama gharama iliolipwa kukomboa wenye mapungufu, waliofanya makosa, wakipoteza uridhi – sadaka ilirejesha vile vilivyopotea. Alisema dunia yote imepotea, na alikufa ili afanyike kuwa sadaka ya kukomboa watu.

**6. Alisema atafufuka tena.**

Alisema atafufuka tena, atakapokufa atafufuka tena kutoka kwa wafu, (kuna zaidi ya hayo, nimechagua machache tu).

Sasa, kama mimi Mchungaji nikitembea kwenye jukwaa hili la Kanisa Kuu na kuchukua kipaza sauti na kusema “Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani,” unaweza kufikiri, labda Mchungaji anataka kunukuu, “mikono yangu imekombolewa na neno la Mungu kuhubiri mamlaka.” Unaweza kusema ladda huyu mchungaji anasititizia mamlaka ya neno analolisoma.

Lakini kama niliendelea na kusema, kama vile naongea na Mungu: “Nipo hapa Baba. Nimefanya yote uliyonituma. Hakuna kasoro, hakuna mapungufu. Sheria hainisumbui mimi, nimeshaitimiza,” na nimeshaanza kukiri ukamilifu kama Yesu, unaweza mtia moyo na kumuonea huruma ukimtizama Bibi. Scott. Na kama nikiendelea kusema, “Uzima wako unategemea kuniweka mimi katika maisha yako na kunifanya mimi Bwana wako,” kwa hiyo nitakuwa nimeingilia au kuonekakana kama “chombo.” Sidhani kama ningepata nilichoweka hapa, na ningekufanya ufikiri kama mimi nina uzima.

Na kama ningesimama kiunadamu na kutegemea kuaminiwa? – “Kabla ya Abramu nalikuwapo. Unajua kabla ya yule mtu aliyetoka katika nchi ya Uru; nilikuwepo, nilimuona shetani akitupwa chini hata kabla ya Adamu kuzaliwa”.”

Na sasa naanza kuongelea kuhusu mbinguni kwa ujasiri kama ule tunaokuwanao tukiongelea nyumbani kwetu. Kama nikisema kochi langu la nyumbani ni la kahawia iliyofifia, na unasema, “umejuaje?”Nitakujibu, “Kwa sababu naishi hapo!” Lakini naongelea kitu ninachokifahamu kuhusu mbinguni! Lakini nyie watu ndani ya duka mnaongea hivyo! Na pia ningeweza kusema mimi ni sadaka ya ulimwengu, halafu, mmoja naomba anisaidie nimuwekee mikono mke wangu kabla “sijafa.”

Na unaweze kutambua kwamba ukiri huu wa kufanya mambo yasiyo ya kawaida ni **wa aina ya mtu kama Kristo tu** ambaye amekuwa akitembea juu ya majukwaa ya historia na ni yeye pekee unayoweza kupata vyanzo vyake. Huwezi kukuta waanzilishi wengine wa dini wakisema maneno haya aliyokuwa akisema Yesu. Buddha hadhani kama alikuwa mkamilifu; alihangaika na roho iliyojulikana kama *tanya*, ambayo ilikuwa na maana ya tama mbaya inayoleta dhambi. Alitafuta njia ya kuachilia hali hii ya kimwili, na hakuna aliyeweza. Akaja kwenye njia nane ambayo ilimpeleka kwenye hali fulani ya ajabu ambapo katika hali hii alipoteza ufahamu wa kutambua asili yake, kama ijulikanavyo, *nirvana*. Na alipotoka katika hali hii, aliwapa wale Wanafunzi wake njia - nane, na alichosema ni, “Imefanikiwa kwangu. jaribu; itafanikiwa kwako pia.”

Hakufikiri kwamba mamlaka yote iko juu yake. Badala yake aliwaambia wanafunzi wake (na kati ya maandiko yake) anasema hakustahili kuwaongoza. Aliwaacha tu wamfanyie kazi yeye. Hakuwa na mawazo ya mamlaka juu yake. Hakufikiri kama alikuwa katikati ya dini za ulimwengu. “Njia hii” ilifanya kazi, njia yake ya mafungu 8. Kama vile wengine wote.

Mohammad hakukifiri kwamba alikuwa mkamilifu. Alikuwa mtume – wa- Mungu. Alikuwa na **maono ya uzima** ambayo yalimvuta mtu wa jangwani, lakini hakuwahi kukiri kwamba alishawahikuwa huko uzima wa milele. Hakufa na kufanyika kuwa sadaka kwa mtu yeyote yule. Alikuwa na mamlaka: Mungu alijidhilirisha kwake kwenye maono. Yesu hakuwahi kuelezea kuwa na maono kama mtume alikuwa alivyosema, “Bwana alisema…” Confucius alikuwa na uchambuzi yakini wa jamii, na alisema kuhusu **uchambuzi wa nje** kama mamlaka.

**Hakuna** viongozi wengine waliowahi kujiweka katikati ya dini za ulimwengu, wakikaa juu ya mamlaka, waliokuwa na ufahamu wa ukamilifu kuhusu wao wenyewe, waliokiri kuwa na uzima kabla na baada ya vipindi vyao vifupi vya kukakaa hapa duniani. **Hakuna** hata mmoja kati ya wa waanzilishi mashuhuri wa dini aliyekuwa na sifa hizi ndani ya ukiri wake. Ndio maana unaweza **kuwaheshimu watu hao** kama “waanzilishi” wa dini.

Tukija kwa Yesu, hapa C. S. Lewis anamuita “Mwanzo Mbadala.” **Aidha** alifikiri haya mambo yalikuwa kweli, lakini alikuwa mpumbavu pia kujua kwamba si rahisi kwa mwanadamu kukiri hivyo, **au** hakuwa mwerevu kufahamu haya mambo hayakuwa kweli, kwa sababu ya ubinafsi wake aliweza kuwadanganya Wanafunzi wake kwa kumwamini yeye, na hicho ndicho kinachomfanya aonekane mbaya. Kwa kumalizia, wale waosema alikuwa “mwalimu mwema **na** mweruvu” wanadhihirisha wazi kwamba hawakuwahi kukutana na Kristo mwenyewe aliyekuwa katika historia.

Kamwe usimtazame Kristo kama mmoja wa waliojiona kama yai la kuchemsha, au usimchukulie kama vile anavyosema yeye ni nani, na kama yeye ni Mungu, hivyo atakuwa mkamilifu, na mamlaka yako ndani yake, na ni kama yu katikati ya dini za ulimwengu, na **alikuwa** na sifa hizo

muhimu za kufa na kufanyika sadaka kwa dunia yote. Alikuwa na maarifa ya uzima, **ata**fufuka (**ali**fufuka) tena.

Huwezi kumuweka Yesu katika kundi la "walimu wema na werevu" na kumsahau. Lazima atakuwa halisi au si halisi, au kile anachodai yeye kuwa.

Vema, nilipofika kwenye njia panda, niliamua kuwa nitapumzika mwenyewe. Kuna jambo lililokuwa likizunguka kuhusu ukweli huu wa historia. Yesua alisema, kwa wale waliotaka ishara, "nitakupa moja." Kuna ishara moja ya mkataba ambayo kwayo imani inaweza kujengwa. Kwa muda mwingine Mungu amefanya zaidi ya mkataba huu, lakini **ishara ambayo Mungu ametuhakikishia** ni kudhibitisha kweli yake ni ishara ya Yona, ikitafsiriwa kama kifo cha Yesu na **ufufuo** wa Kristo.

Kwa wakati fulani katika mtiririko wa historia ujumbe wa KWELI unaibuka. Mungu aliamua kuingia katika hema ya mwili wa mwanadamu, kutimiza sheria iwe kitu cha binafsi, anaamua kufa badala yetu kama sadaka ya ukombozi, kama ilivyojulikana kama kutimiza kwa sheria ili afufuke na kutuingiza katika familia yake ya maisha mapya bila ya mzigo wa sheria, hivyo ndivyo ilivyokuwa kama mwalimu wa shule kutufundisha sisi mahitaji au umuhimu wa nguvu ya Mungu ya ukombozi.

Hivyo aliingia katika jukwaa la historia ili kutangaza Ukristo, na alijithibitisha mwenyewe kuhusu KWELI ambayo inaweza kuelezeka.

Sasa UKWELI ni kwamba hakuna historia iliyo na uhakika. Nilijifunza hivyo nikiwa nachukua shahada yangu ya historia, "Historia ya Uhakiki" imaanishayo kwamba kila kipengele cha **mapokeo** ya ushahidi kipo pale. Ambacho unaweza **kupokea** kama ushahidi ni lazima kiwe na uhakika wa kihistoria. Ikiwa tukio limepita tu, na umepoteza uwezo wa kuwa naushahidi. Kamera zinaweza kusaidia, lakini hapo lile jambo linakuwa limeshapita. Kitu tu unachoweza kutumainia ni uhakika wa kisaikolojia, ila ni pale tu lile jamba la kihistoria linakuwepo kukupa mwitikio kisaikolojia, na huo mwitikio ni vigumu kuwanao.

Wakili yeyote mzuri anajua kwamba mahakamani hakuna kitu anachosema wakili na kisha jaji kumkemea, wakili anajua hata kabla hajaongea kwamba anachotaka kukisema hakutakiwa kukisema, ila anataka jopo la majaji kumsikia. Na jaji anapiga kelele, na kusema, "Ndio, mheshimiwa," na anafanya hivyo kwa upole. Anajua kitu halisi anachokifanya. Hapo jaji atazama jopo la majaji na kusema, "tupilia mbali hilo shitaka". Anagonga mlio! Hii ndio njia pekee anayoweza kutumia kutupilia mbali shitaka. Na unaona, unasikia, na kuhisi, ushahidi mwingine unaoweza kuwepo.

**Mungu Alimthibitisha Mwanae Kwa Ufufuo.**

Paulo anakuja kwenye kilima cha Mars; wanafalsafa wanakutana pale kufikiria miungu wengine wote, kwa hiyo wanaogopa wasije wakamsahau mmoja wao ambaye ana kumbukumbu za Mungu Asiyejulikana. Anatumia nafasi hiyo kumjadili Kristo. Anasema, "Nitawaambia huyu Mungu Asiyejulikana ni nani," na anamuhubiri Kristo, ambapo anasema Mungu alimtangaza kwa Ufufuo. Paulo anaema kama hakuna ufufuo, basi imani yetu ni bure, na sisi tu mashahidi wa uongo wa Mungu, na tumemshuhudia yeye aliyemfufua Kristo.

Ujumbe wa kwanza wa kanisa ulikuwa ni ule wa Petro aliohubiri katika siku ya Pentekoste, "Huyu ndiye Yesu mnayemfahamu …" Nalimtaja kwa sababu alijua wanafahamu kwamba alisurubiwa: na ya kwamba hilo wanalifahamu. Halafu akashuhudia kile ambacho hawakifahamu. " Huyu Yesu aliyefufuka ambaye sisi sote tu mashahidi wake," na kutanguliza hiyo kweli iliyothibitika. Paulo katika moja ya hotoba zake anasema,  " Yesu alionekana, alionekana," na anorodhesha shuhuda zake na anukuja kwenye kundi la watu na kusema, "… kwa mara moja kwa watu zaidi ya mia tano.

Katika siku hizo ungeweza kukusanya mashahidi; sio leo. Lakini sio kwa jumbe nyingine za kistoria, kuanzia yule aliyeandika Shekespeare mpaka Kaisari Julius, unaweza kutafuta UKWELI wa kihistoria kwa kuangalia misingi ya kikristo inayojulikana kama:

**Yesu alitoka Kaburini.**

Nitasema hivi kuweka mfano huu. Kama mtu yeyote anayesikiliza akija katika Kanisa hili kuu akidai kuwa Yesu alijiumba mwenyewe, nitatoa ushauri kwamba aende kwa wanasaikolojia na kwenda hospitali, labda nione mng'aro wa macho yake ya kwamba walikuwa wananidanganya,  kwa sababu mwanadamu anadai hivyo. Lakini kwa madai kwamba mtu anasema hivi " Nizike na katika siku tatu nitafufuka kutoka kaburini na kuonekana."  Na katika zile siku tatu mtu huyo huyo anafufuka kutoka kaburini, ningemtazama kwa mtazamo mwingine huyo mtu anayedai hivyo. Sihitaji kitu kingine chochote kama msingi wa imani; sihitaji falsafa nyingine tena za kimaandiko. **Huyu aliyefufuka, kama ikiwezekana awe na mwanzo wangu wa uhusiano na Mungu wa kweli**.

Kama kwenye jukwaa la historia ninaweza kumpata yeye yule ambaye maneno yake ninaweza kuyatumia maishani mwangu kufanyia utafiti, ya kwamba nani alikuwa mkamilifu, aliye katikati ya mamlaka, katikati ya dini za ulimwengu, na vitu vyote hivi vingine, na ukiongezea kunikomboa mimi, aliyefufuka na kuandaa makao ya milele, huyu ndiye Mungu ninayemuhitaji. Ninaanzia hapo hapo.

**SOMO: ALIFUFUKA KUTOKA KABURINI?**

Huwezi kumaliza kwa kudhani hivyo; lazima utafiti. Kutafiti kitu lazima uwe na **misingi ya kweli**. Watu wengi wana mawazo yasiyo ya uhakika, wanabisha kwamba ufufuo haukutokea lazima ni uwe muongo. Ukweli mwingine wote unaweza kuutafiti.

Kama ukiuliza, Scott aIihubiri ujumbe wa muda wa saa moja Jumapili? Unatakiwa ufikiri kwamba nilikuwa pale na nilihubiri. Lazima ufikiri kwamba Kanisa Kuu lipo. Pia lazima ufikiri kuwa Jumapili hiyo ilikuwepo na ikapita. Hatuna haja ya kushauriana kuhusu hilo; tunachukulia vitu hivyo kiujumla kama tukiona huo ujumbe ulikuwa wa saa moja (au zaidi), hebu kwanza tukubaliane kwamba nilihubiri. Huna sababu ya kukubali kwamba mahubiri yalikuwa mazuri au mabaya, lakini nilikuwepo na nilifumbua mdomo wangu na kusema kitu. Hicho ndicho kinachojulikana kama mfano wa kuangiliwa – unaochuliwa kiujumla.

Kama mtu akisema, "siamini kama ulikuwepo", kasha akanyamaza huku akiwa na maswali mengi kichwani. Ni rahisi kuhakikisha kwamba nilikuwepo kuliko kuhakikisha kwa gain muda  nilihubiri, kwa sababu hujui ni muda gani nilianza. Je ulikuwa mwanzo wa habari? Ulikuwa mwanzo wa ishara?

Hili linaonekana kuwa na marumbano kiasi, kuhakikisha kwamba nilikuwa pale au la hasha, lazima uhakikishe, hii ni rahisi kidogo.

Unatakiwa kuutazama ufufuo kwa jinsi hiyo. Kuna baadhi ya kweli ambazo unatakiwa ufikiri kabla ya kuelezea ufufuo. Ya kwanza ni kuwa, Yesu alikuwepo? Kwa nini tunaongelea kwamba alifufuka kama hatuamini kuwa alishakuwepo? Kuna nyakati kulikuwa na marumbano; sio sasa tena. Kwa kusudi la leo na majadiliano yoyote ya ufunuo, lazima angalau ufikirie mambo haya:

**Kweli ya 1. Yesu Aliishi.**

Kama huamini kwamba … Unakubali kuwa ni rahisi kuhakikisha kwamba Yesu aliishi mahali fulani wakit fulani kuliko kuamini kwamba alikufa na kufufuka tena? Unaamini hivyo? Hivyo unaweza kunipa kazi rahisi. ‘’ Vema, sina uhakika kama aliishi, hivyo naomba usinipe maelezo ya ufufuo.” Sina muda tena wa kufanya vitu vingine zaidi ya hivyo. Usijiingize kwenye malumbano na mtu yeyote ambaye haamini kwamba Yesu aliishi/alikuwepo. Hiyo ni rahisi sana kuthibitisha, mpaka hiyo ikubalike, usiache mjadala mwingine tena:

**Kweli ya 2. Alisurubiwa kwenye mbele ya viongozi fulani wa dini ya Kiyahudi kule Yerusalemu. Mamlaka za Kirumi ndizo zilizoamrisha na kuendesha mashitaka.**

Katika mwanzo huo viongozi fulani wa Kiyahudi, (sio Wayahudi wote waliolaumu, Wanafunzi wake walikuwa Wayahudi, ni viongozi wachache tu wa Kiyahudi), Warumi waliendesha mashitaka. Kama usipoamnini hivyo,hakuna sababu ya kuongelea Ufufuo. Kusurubiwa ni rahisi sana kukuhakisha kuliko Ufufuo.

**Kweli ya 3. Ya Kwamba alidhaniwa amekufa.**

Angalia nasema alidhaniwa kuwa amekufa, kwa sababu watu wachache waliamini alitoka kaburini – amefufuka. Alidhaniwa amekufa: alichomwa na upanga, akashushwa chini kutoka juu ya msalaba, akawekwa kaburini. Bila shaka, moja ya wananadharia alielezea jambo hili jinsi Yesu alivyofanyiwa, na watu walimpleka kwenye kaburi na wakijua kwamba atafufuka. Alilifanya kwa Lazaro kwanza (hiyo ndio nadharia yenyewe) lakini kwa sababu Lazaro alikuwa akinuka kabla ya kufanya hivyo. Baadhi ya nadharia nyingine zinataka ufikirie sana ili kuzielewa kuliko tu kukubali huo Ufufuo, lakini angalau Alidhaniwa kuwa amekufa. Kama huamini hilo, kujadili Ufufuo kwako ni kitu cha kitoto.

**Kweli ya 4. Alizikwa kwenye kaburi lililojulikana na kufikika.**

Watu wa nyakati hizo ha hasa viongozi wa Kiyahudi na Kirumi walishiriki katika tukio la kumsurubisha Yesu, walijua kaburi liliko na wangeweza kufika huko. Usingeweza kufika huko kwa sababu ya miamba na walinzi, lakini kaburi lilikokuweko kulijulikana na kulifikika.

**Kweli ya 5. Kisha Alihubiriwa kuwa Amefufuka.**

Hata sasa siwezi kusema alifufuka, lakini **alihubiriwa** kuwa amefufuka, na hilo kaburi lilikuwa wazi, na Yesu alipaa. Ni vizuri kukumbuka kwamba mahubiri yote yamejumuisha: ya kwamba kaburi li wazi; amefufuka katika wafu; amepaa mbinguni. Hayo mambo yote matatu yalihubiriwa.

Sasa, kama huamini Alihubiriwa katika mambo hayo yote matatu, ninafanya hayo yote leo. Lakini alihubiriwa **mapema katika mji ule ule** ambao aliouwawa! Kam huamini hivyo (basi mtiririko mzima wa madai haya kwamba alihubiriwa), ni rahisi kuthibitisha kuliko Ufufuo.

**Kweli ya 6. Viongozi wa Kiyahudi waliochochea kusurubiwa kwake walikuwa na nia ya kukanusha Ufufuo wake kuliko kama tungefanya hivi leo.**

Akili ya kawaida itakuambia viongozi wa Kiyahudi waliochochea kusurubiwa kwakwe, walikuwa na nia ya kutaka kukanusha Ufufuo kuliko mtu aliyeondolewa miaka 2,000, wakifikiria jambo hilli kitaalamu huku wakiwa na kutoamini ndani yake, kwa sababu sifa za viongozi wa Kiyahudi ilikuwa sambamba na maisha mazuri, kama vile mkate usivyoweza kuachana na siagi. Kama walichochea kusurubiwa kwake, kwakimshutumu kwa kutaka kuanzisha ufamle wa kizazi cha wasio haki, na ghafla tu ni kwamba alikifufuka kotoka kwa wafu, watakuwa wanaanza kutafuta kazi mpya. Kwa hiyo kwa akili ya kawaida unaweza kusema kuwa walikuwa na lengo la kukanusha hili jambo, na wangejiweka mbali na watu wengine siku ya Jumapili ya Pasaka.

**Kweli ya 7. Wanafunzi wake waliudhiwa kwa sababu ya kuhubiri Ufufuo wake.**

Waliudhiwa vibaya sana kwa sababu ya haya mahubiri, kuanzia hao viongozi wa Kiyahudi, ambao mwanzo waliwaudhi, kwanza waliwaita wao kuwa ni waongo, pili walisema wameiba mwili wa Yesu. Kitabu kizima cha Matendo ya Mitume kinaezea jinsi Wanafunzi wake walivyoudhiwa kwa kuhubiri Ufufuo.

Baadaye, karne zilizofuata, Kwa ujumla Wakristo katika Dola ya Kirumi walikuwa wakiwindwa kwa kufanyiwa mabaya na wakalaumiwa, na wakaadhibiwa kwa sababu nyingine sisizo zao, lakini kila kumbukumbu inakubaliana na **unyanyasaji wa awali** kwamba ungekoma tu pale ambapo Wanafunzi hao wangeacha kuhubiri ujumbe wa Ufufuo, na kupaa kwa Yesu. Ndiyo maana waudhiwa, kwa sababu viongozi wa Kiyahudi walikuwa na majina makubwa kwenye jamii.

**Kweli ya 8. Kaburi lilikuwa wazi.**

Haya yote yanaelekea kwenye ukweli, utashi wa kawaida unasema, kama viongozi wa Kiyahudi waliochochea kusurubiwa (Kweli ya 2), walikuwa na malengo yao mengine kwa sababu mapato yao yalikuwa katika hatari (kweli ya 6); na kama angezikwa mahali palipojulikana, panapofikika (Kweli ya 4), wangekwenda mara moja kaburini na kuutambua mwili. Kwa hiyo ni wazi kwamba kaburi lilikuwa wazi.

Kaburi lilikuwa ni kitu cha bure kwa sababu lilikuwa wazi! Karne ziliyoyoma na kaburi lilipoteza historia, kwa sababu hakukuwa na mtu ndani yake! Kisha, ‘’Kipindi cha historia’’ kilianza kukua,

watu walianza kuwa na mapenzi juu ya kaburi la Yesu, ambapo mwanzo hawakuwa na mapenzi kwa sababu hakukuwa na mtu ndani yake, na walijitahidi kumtafuta.

Na kanisa lote linapigana hivi leo juu ya sehemu za kale za kihistoria za makanisa, na kaburi la Gordon ambalo waprotestanti wengi wanajitambulisha kwalo, baada tu ya kituo cha basi chini ya kilima kilichoitwa ‘’Golgota’’ ambapo juu yake pana makaburi ya waarabu. Mapigano hayo yalitokea kwa sababu kaburi lilipoteza historia yake; hakukuwa na mtu ndani yake.

Sasa, kweli hizi ni rahisi kuzielezea kuliko Ufufuo, lazima kama kweli hizi zitakubalika, hauwezi kuelezea nadharia zote juu ya Ufufuo. Kwa mfano, mahubiri yamewawafikia walengwa na kwamba kwa karne zote watu wamekuwa wakieleza nadharia kufafanua jambo hilo. Sasa, kwa sababu hiyo kila pasaka najitahidi kuelezea ili kwamba uelewe unapokuja kanisani, uchambuzi wa kutumia akili yako inahitajika pia.

Huwezi kuwafanya watu waamini, lakini ukiweka wazi ushahidi, kitu fulani hutokea ndani yake na kutakuwa na mwitikio wa kisaikologia. Ugomvi wangu na watu wanokataa Ufufuo na wanaishi maisha yasiyoangalia huo Ufufuo, ni kwamba ninaweza kuuliza maswali 15 na utakuta kuwa hawezi kutumia masaa 15 ya maisha yao kutafuta ushahidi wa hilo jambo.

Kama Ufufuo ni kweli, hivyo ni kiini cha ulimwengu. Kama Ufufuo ni kweli, hivyo ni kiini cha ukweli wa kihistoria. Unatakiwa kuwa mpumbavu kati ya upumbavu wote wa kibinadamu kufikiri kwamba haina thamani angalau kwa masaa 30 kujifunza maisha yake. Zaidi, kuna watu wengi duniani wenye akili nyingi wameliangalia jambo hili na kushawishika. Ndiyo maana nafanya hivi. Kwa sababu mahubiri ya Wanafunzi wake ni ya kweli, nadharia zote zinaelezea imani, lakini nadhria hazikielezei kama ukiangalia zile kweli nane nilizozielezea hapo awali.

**Nadharia ya 1. Wanafunzi wake waliiba mwili.**

**Nadharia ya 2. Viongozi wa Kiyahudi waliiba mwili.**

**Nadharia ya 3. Viongozi wa Kirumi waliiba mwili.**

**Nadharia ya 4. Wanawake walikwenda kwenye kaburi lisilo lake.**

Unajua, ilikuwa giza na walipita kama ‘’wanawake – watembezi’’ hawakuwa wanawake madereva, lakini walikuwa wanawake watembezi. Walikwenda vibaya kwenye kaburi, na waliamini ameshafufuka, na nina maana walikimbia huku wakilia nje ya bustani, ‘’tumekwenda na hakuwepo. Walikwenda kwenye kaburi lisilo, walikwenda kwenye kaburi lililo wazi,, wakisubiri mtu mwingine tena.

**Nadharia ya 5. Yalikuwa ni maono.**

Ndoto za mchana zenye utukufu. Kwa sababu walikuwa wakweli; waliamini kwamba hiyo ilitokea kwa sababu walikuwa na maono haya.

**Nadharia ya 6. Nadharia ya marejesho.**

Alisurubiwa na alidhaniwa kuwa amekufa, na alizikwa katika kaburi lisilijulikana, lakini katika hali ya utulivu wa makaburini alifufuka na akatoka nje ya kaburi akiwa ndani ya sanda, ashukuriwe Mungu kwamba walinzi walikuwa wamelala, na alillsukuma liwe jiwe kando ya njia – na akawa kama Frankenstein!

**Nadharia ya 7. Wanafunzi wake walidanganya.**

Alifanya jambo lile kuwa jipya. Walifikiri vibaya na hawakuweza kukaa na hilo jambo kwa hiyo walitunga hadithi yote na iliwachukua wiki saba kuitengeneza, na kisha waliisimulia.

**Nadharia ya 8. YOTE NI HALISI.**

Waongolea kitu halisi walichokipitia na walichokiona. Sasa, kama ulivyoelewa "mwanzo mbadala" ulivyomfikiria Yesu pekee katika historia, kwamba aidha kichaa, punguani, mnafiki, au alikuwa kama alivyokuwa, na hii inahitaji maelezo au maana ya uungu, ili kuwa na "mwanzo mbadala."

Nadharia hizi zote zinajitegemea. Hata nadharia ya kwanza (Wanafunzi waliiba mwili wake), ambao viongozi wa Kiyahudi waliiunda wenyewe. Lakini nadharia hii yenyewe inakulazimisha kuwashitaki Wanafunzi kuwa ni waongo. Hivyo, unalazimika tena kuangalia "mwanzo mbadala.''

Ninachukia – na nimekuwa nikichukia hili jambo nilipokuwa nikichukua shahada yangu ya historia – Ninachukia mwana historia anayejihesabia haki: "Nina malengo; Sijali maoni." Hakuna kitu kinachojulikana kama mtu mwenye ufahamu ambaye hajali maoni; hamna uzoefu katika kweli unaokufanya uwe vile vile. Maarifa yanajenga mawazo, ukijifunza kweli hizo zilizoorodheshwa hapo juu kuhusu Yesu, njia mbili tu ndizo zitaruhusiwa. **Aidha** Wanafunzi wake walidanganya **au** walielezea ukweli. Hebu tuchuguze kila Nadharia na tufanye maamuzi:

**#1 Waliiba mwili** (Nadharia ya 1), ni hakika walidanganya (Nadharia ya 7).

**#2. Viongozi wa Kiyahudi waliiba mwili** (Nadharia ya 2)? Kweli hizi zinapinga kwamba: walikuwa na lengo zaidi la kupinga mahubiri (Kweli ya 6), kwa sababu hiyo walilifanya kaburi kuwa wazi? Na kama walilifanya hivyo, wangesema, "Subiri dakika; tuchukue huu mwili kutoka kaburini." Wasingeweza hata kufikiri hiyo hadithi; walimuelezea yeye kuhusu wanafunzi wake (Nadharia ya 1), hata kama ilikubalika, wanafunzi wake hawakuhubiri tu kaburi lililowazi bali na Ufufuo pia. Walimhubiri Yesu aliyeonekana na kuishi, na yule ambaye walikula naye chakula; walihubiri kupaa kwa nguvu zao zote. Hivyo hata kama kule kuchukua mwili kwa viongozi wa Kiyahudi kulielezea kaburi kuwa wazi, wanafunzi bado wanasimulia mambo yaliyotokea kwenye mwili uliofufuka na kupaa, hivyo wamekuza na kutunga hadithi nyingi – kwa maneno mengine **wamekuwa wakiendelea kudanganya.**

**#3. Viongozi wa Kirumi waliuchukua mwili** (Nadharia ya 3)? Pamoja na malumbano hayo kule Yerusalemu, pamoja na ukaribu wa viongozi wa Kiyahudi waliokuwa nao na viongozi wa Kirumi, kulikowawezesha kukamilisha kusurubisha, usifikiri kwamba waliuweka wazi ukweli, kwamba

maafisa wa serikali ya Kirumi waliuchukua mwili? Lakini kama hilo linaelezea kaburi lililokuwa wazi, haiwaondolei wanafunzi wake kazi yao ya kuhubiri mwili uliofufuka waliokutana nao, na kupaa kwake, kwa hiyo bado wanadanganya.

**#4. Wanawake walienda kwenye kaburi lisilo** (Nadharia ya 4)? Lilikuwa kaburi lililojulikana na kufikika (Kweli ya 4). Nia ya viongozi wa Kiyahudi (Kweli ya 6) ingewapeleka kwenye kaburi lillilojulikana, walitakiwa waelezee nadharia ya uongo ya kaburi ilikuwa waende kaburini ambako mwili ulikuwepo – wangefanya hivyo.

**#5. Maono** (Nadharia ya 5)? Vema, kaburi li wazi (Kweli ya 8) inaelezea hivyo. Kama yangekuwa maono, kungekuwa na mwili ndani ya kaburi. Lazima ungekuwa ni mwili uliotengenezwa. Kwa hiyo wanadanganya.

**#6. Marejesho** (Nadharia ya 6)? Vema, Frankenstein kutoka kaburi haimaanishi kwamba Yesu aliyekuwa anahubiriwa ni mwema. Lazima ielezee kaburi lililo wazi, lakini haielezei aina ya Yesu waliyemuhubiri, hailezei kupaa – bado hiyo hadidhi waliitingeneza tu.

Kwa hiyo hata kama ukiangalia hilo, ukaangalia na kweli nane ambazo ni rahisi kuelezea kuliko hata Ufufuo, kuna njia mbili tu, mwisho wa aina mbili, kwa sababu zinaelezea wazi ukweli wa ushahidi. Ndiyo maana siwajali wanaopinga Ufufuo na hawajasoma kabisa kitabu kinachojulikana kama, *Sherlock's Majaribu ya Ushahidi.* Amelezea picha ya mahakani ambapo mashahidi wake wote walikusanyika na wakatoa ushahidi wote wa mahakama ya Kiingereza. Au, hawakusoma *Ni Nani Aliyeondoa Jiwe?* Kitabu kilichotungwa na wakili ambaye alipinga Ufufuo na akaishia kuandika moja ya mijadala ya ushawishi.

Unakumbana na "mwanzo mbadala": **aidha NJIA YA 1** (ambayo ni Nadharia ya 7): hawa wafuasi walitunga hadithi kuondoa aibu na ilikuwa ni uongo, **au** **NJIA YA 2**: **Wanaelezea kama watu wakweli kitu halisi kilichotokea.**

Sasa, kama una matatizo ya kutofautisha kati ya "Kweli," "Njia Mbadala" na "Nadharia," ngoja niweke sawa jambo hili: Kuna kweli nane ambazo zimepunguza nadharia nane kuwa nadharia ya 7 na 8 tu (zenye mianzo mbadala), na kisha zikawa nadharia mbili za kueleweka, hivyo zikaleta mbidadala miwili, "Nadharia" ya 7, walidanganya, au ya 8, walisema kweli!

Na tukija hapo, tunaona kwamba imani yote ya Kikristo inazunguka kwenye jambo hili: Hawa Wafuasi waliokuwa mashahidi wa kweli wanaongea kitu walichokiona, au wazushi waliodanganya ili kuondoa aibu? Hizi ni sababu nne zinazonifanya nione kuwa hawakuwa wanadanganya:

**Sababu ya 1. Dhoruba yabadilisha ushahidi kuwa kitu kizuri.**

Kila mtu anaamini kuwa Petro hakuwa imara, hata walipokuwa katika kundi asingeweza kuhesabiwa kuwa angasimama.Alikuwa na hofu na alimkana Bwana wake, kila mara alikuwa kwenye misukosuko hii ni kwa sababu ya hofu yake kubwa na kutokuwa imara. Baada ya Ufufuo, ni mtu aliyehubiri kwenye makundi yenye utani, alitimiza hatma yake kuwa ni Mwamba, alikufa kwa ujasiri akidai awekwe kichwa chini juu kwa sababu hakuwa na thamani kufa kifo alichokufa Bwana

wake – dhoroba hiyo yenye mabadiliko inajulikana mpaka leo kwenye historia, na hiyo historia ni mwanzo wa hadithi za Ufufuo.

Yohana? Alikuwa mbinafsi. Alikuwa mmoja ya watu walojulikana kama "Wana wa Radi." Alitaka kuita moto kutoka mbinguni kwa kila mtu aliyempinga. Yeye na kaka yake walimtumia mama yao kutafuta ufalme wa mbingu. Baada ya hadidhi ya Ufufuo, kila mwandishi alikubaliana na Yohana kwamba ni mtu aliyebadilika. Badala ya "Wana wa Radi," alikuwa mdhaifu licha ya muonekano wake upendo wa kutoshidwa. Alijulikana kama "Mtume wa Upendo" – mabadiliko makubwa ya dhoruba.

Tomaso alikuwa mtu wa mashaka: kuanzia mwanzo mpaka mwisho, ni mtu mashaka. Ni mnyenyekevu; anauliza kila kitu. Yesu anapokwenda Samaria kukutana na kifo, anawaelezea wanafunzi wake kuhusu hili jambo, "Twendeni na sisi, tukafe pamoja naye." Huo ni ujasiri, lakini alifikiri Yesu angekufa; huu ni uungwana.

Yesu alipokuwa akijadili kuondoka, kujenga makao mbinguni, alisema, "mnajua kama nakwenda, na njia mnaijua," na wengine wote walishangilia kuhusu ufalme wa mbinguni. Tomaso anashangilia kila jambo. Anasema "Hatujui uendako: twawezaje kujua njia" Sasa, hiyo ni mojawapo sifa ya ijulikanayo kama thumbnail.

Ni nani aliye na mashaka Ufufuo unapokuja? Ni yule yule. "Siamini mpaka nimguse, niweke mkono yangu kwenye alama za kifo. Muda ulipowasili. Yesu alikuwa pale anamwambia Tomaso, "Tazama mikono yangu na mbavu zangu. Alisema", "Ni heri kuamini kuliko kuona,". Yesu yule pale, na anamwambia Tomaso," Huu ni ukweli wa wazi wazi, lakini hakumlaumu Tomaso. Alisema tu ukweli, na akatoa mtihani, ambao ni huu tunaoufanya sasa. Alisema, "Tazama mikono yangu na mbavu zangu." Na Tomaso alilia, "Bwana wangu na Mungu wangu."

Ni muhimu kwamba maeneo mengi ya kifalsafa ya duniani, ambapo falsafa ya Vedanta imeleta Ubudha na dini za Mashariki ambazo zinatokana na hiyo, ni Tomaso aliyepenya milima ya Himalaya kujitoa mhanga karibu na Madras, India, na kuwa mwalimu/kiongozi wa imani katika eneo moja la dunia lenye changamoto kwa wakati ule, na hakuwahi tena kupinga imani ya karibu – ni mabadiliko kutoka kwenye mtu wa mashaka kwenda kwenye "mwamini" asiyetikisika.

Na sasa, unaweza kusema, msukosuko unaweza kubadilisha watu, lakini uongo hauwezi kubadilisha watu kuwa wazuri, watazidi kuwa wabaya. Hawa watu kwa bahati mbaya wamekuwa wazuri, sifikiri kama kusema ukweli kutawabadilisha.

**Sababu ya 2. Ushahidi usio wa moja kwa moja na makubaliano ya ndani.**

Kuna ushahidi wa ukweli usio wa moja kwa moja. Marko aliwaandikia Wayunani; unaweza kuhesabu Injili ya Marko, anamuelezea Kristo zaidi kama "Mwana wa Adamu" kuliko Injili nyingine. Hesabu mwenyewe.

Sasa kama alikuwa muongo, jua kwamba alikuwa akidanganya, kujaribu kupenyeza uongo, kwa nini alimuelezea Yesu kwa kutumia maneno ya upole kama nia yake ni kumuonyesha Yesu kama ni

Mwana wa Mungu? Kama alikuwa muongo, asingemuelezea Yesu kuwa ni Mwana wa Mungu. Lakini kwa kawaida tu, kama ushahidi mdogo wa ukweli wa siri wa Mungu, katika kitabu cha Marko, aliwaandikia Wayunani, akilenga kuthibitisha kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, alimuelezea Yesu alikijita Mwana wa Mungu kuliko Injili nyingine zote.

Sasa, Yesu alijiita mwenyewe kama “Mwana wa Adamu,” kwa sababu Yesu alikuwa akihubiri kwa hafla ya Waebrania ukisoma kitabu cha Enoki na ukisoma kitabu cha Danieli ambapo Mwana wa Adamu ameonekana kama Masihi anayekuja katika mawingu ya utukufu kuleta ufalme wake. Kwa hiyo ni hakika kwamba Yesu asiyejua lolote kuhusu Agano la Kale alijiita yeye kama mwana wa Adamu kwa mtazamo wa kimasihi, lakini kama unawaandikia Wayunani wasiojua lolote kuhusu Agano la Kale, na kujaribu kupenyeza uongo wa kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu utakuwa mkweli, hutakuwa na Yesu anasema “Mwana wa Mungu” mara kwa mara. Kwa nini usibadilishe anachosema kutimiza lengo? Ukweli wa asili. Ninaweza kukupa dazani ya hayo, lakini hivyo ndivyo wanahistoria wanaita ushahidi wa wazi usio wa moja kwa moja.

Njoja nikuongezee nyingine tena. Katika dunia ya Agano Jipya, wanawake walidhaniwa kuwa hawawezi kuwa mashuhuda wazuri. Wanafunzi wake walijua hivyo, kwa hiyo kwa nini waliwaweka wanawake kama mashahidi wa kwanza wa Ufufuo? Kama walikuwa wanasema uongo, wangejua kwamba dunia yao isingeujali ushahidi huu wa wanawake. Waongo wangepinga kuweka kumbukumbu za wanawake hawa. Ushahidi mwingine wa kweli ni kwamba walitoa ripoti ya mambo halisi yaliyotokea.

Ukweli kwamba Wanafunzi walisubiri wiki saba unatumika kwa wasemao walikuwa wakidanganya na kama muda ulivyowahitadiji kuupika uongo. Kama wangekuwa na akili kudanganya uongo huu, hukumu yangu ni, wangechunguza. Walisubiri wiki saba kwa sababu Yesu aliwaambia wamsubiri. Hiki ni kitendo cha mtu muwazi, hata kama kusubiri kwa muda wote huo hadithi yao – kama wangekuwa wanatunga uongo.

**Sababu ya 3. Gharama ililipwa.**

Haulipi gharama hizi walizolipa watu hawa kusema uongo. Wote, walimuokoa Yohana aliyekufa kifo cha kujitoa muhanga: Bartholomeo alipinga kifo cha kipigwa kwa mkanda kule Amenia; Tomaso alikatwa na upanga wa Brahmin; Petro alisurubiwa kichwa chini miguu juu, Mtakatifu Andrea alisurubiwa kwenye msalaba wa Mtakatifu Andrea (ndiko jina hilo lilikopatikana); Luka alinyongwa na makuhani wenye kuabudu miungu wengine, Marko aliburuzwa katika mitaa ya Alexandria mpaka kufa. Hawa watu walilipa gharama zaidi ya kawaida ya kibinadamu kwa “uongo” wao.

**Sababu ya 4. Walikufa peke yao.**

Mtakatifu Tomaso Aguinas – mkuu, nafikiri kithibitisho cha ukweli wa wanafunzi wa Yesu na Ufufuo ni kwamba walikufa peke yao. Sasa, nafanya kila mwaka nikimaliza ujumbe huu, ninaweza kuunda kundi la watu wanaojaribu kujificha aibu zao, kusimulia hadithi, kukisia mtu asiye yule, aliyeshidwa (wangeangalia hilo), akijaribu kumshinda yeye kwa uongo.

Ninaweza kupata picha yao wakiwa pamoja na ushawishi wa kimakundi wakiendelea na uongo wao, kwa sababu hawataki kuwa wa kwanza kuangusha imani na kuwaegemea wenzao na kuangusha kitu chote.

Ngoja tuanagalie ile hadithi ya kutungwa ya Bobby Boyle na Jerry McIntyre na Richard Williams. Huna runinga, huna satelaiti, huna faksi, huna simu, na kama unaishi pamoja na migandamizo mikubwa, hautaki kuwa yule mojawapo, kumuangusha Richard na Bobby.

Lakini sasa jitenganishe. Wewe, Jerry, uwe Bartholomeo wa kule Armenia; na wewe, Bobby, uwe Tomaso kule India. Na Richard, awe Petro wa Roma. Mpoteze mawasiliano ya kila mmoja wenu. Unaweza kunyanyua simu na kumpigia mtu yeyote; hakuna ajuaye ulipo, kwa sababu unajua unadanganya, na unajua hakika usitegemee kamwe kuamini hivyo, na wewe, Jerry, kule Armenia, unapigwa na kufa, kwa kweli – hivyo ndivyo, unachunwa ngozi kwa mijeredi, ngozi yako inachunika – unachotakiwa kufanya ni kusema, "Ni uongo," na Mnisamehe; Ninauhama mji."

Bobby asingejua hilo; Richard asingejua hilo. Angeweza kumuona mara nyingine, wakisimuliana hadithi na kusema, "Kijana, nimewachakaza wote kule Armenia. Nilisimulia hadithi, na hakuna mtu angeweza kusahau hilo na jinsi nilivyoisimulia," Bobby na Richard wasingejua kama nadanganya.

Wewe Bobby, utakatwa upanga India; hutawaona Jerry na Richard tena. Unachotakiwa kufanya ni kuondokana na msongo ni kusema, "Ni uongo."

Wewe, Richard, uko Roma; uko katika madhara zaidi, na maisha yako yako mikononi wa watu wazito, unachotakiwa kusema, Samahani. Labda nimeota, nakunja na naelekea Ufaransa.

Kama Tomaso Aquinas alivyosema, kisaikolojia haikubaliki kuwa watu hawa, walijitenga, kila mmoja akilipa gharama ya juu kwa simulizi zao na kila mmoja kufa peke yake, na baadhi yao katika kundi wasingeachana na kusema, "Jamani, haikuwa kweli!"

Kufa peke yako. Na ushahidi usibaki miaka 2,000 ya kupingwa kwa hali ya juu, hauwezi ukapata kumbukumbu popote hapa duniani ambapo yeyote yule kati ya watu hawa waliopinga mpaka kifo wakisimulia hadithi hii. Kwa hiyo, ninakuja kwenye hitimisho kwamba hawa watu hawadanganyi. Walikuwa wakisimulia walichofikiri na kupitia na kuona kama ni kweli.

Nakumbuka hivi nikiwa na Profesa Larry Thomas pale Stanford, aliniambia, "Gene, ninashawishika. Hawa watu waliamini walichokisimulia. Kwa hiyo, baadhi ya kweli hizi nane lazima zitakuwa za uongo. "Vema, kama ni mkweli na unasema hivyo, nimekupata, kwa sababu hizo kweli nyingine nane ni nyingi kuzihakikisha. Ni nini mbadala?

**NI KWELI, ALITOKA KABURINI.**

Vema, kama ni kweli, sasa je? Yaliyobaki yote ya huu ukweli, na nina mwanzo wa imani kwa Mungu milele. Na sasa, nimeshavuka kile kipingamizi ambapo ninaweza kutafakari Ukristo ni nini, na kama ninaamini kwamba Yesu Kristo alitoka kwenye zile sanda, kupitia kwenye mwamba, kupitia kwenye ule mlango, na akapaa mawinguni, kasha kuhamishwa kwa zile molekiuli si kitu

kwake – Anaweza kufanya bila kuleta mlipuko. Ni kweli kwamba vitu vyote viliumbwa katika yeye, na anaweza kuvidhibiti.

Kwa hiyo, si vigumu kuamini kabisa kwamba kile kile kitu cha Mungu, kiliwekwa kwa Maria, na kikaja kama Yesu wa Nazareti kupitia Roho Mtakatifu. Mungu anasema ameweka kile kile kitu cha Mungu ndani yetu tukimwani yeye. **Huu** uzoefu kamili wa kuzaliwa - mara ya pili, mwanzo wa maisha, marejesho, kiumbe kipya kinachopenya katika muundo wa chembe chembe za mwili na kuwekwa ndani yangu kama zawadi kutoka kwa Mungu kama nikimwamini kupitia neno lake.

Mwanzo wa Ukristo wote, umeonekana vizuri, kwamba Kristo ndani yetu kama tumaini la utukufu. Sitakiwi kuwa wa kiroho sana au wa kisasa sana kuelewa Ukristo ni nini. Ninaweza kutumia maisha yangu kutenda au kufuata maneno yake, pamoja na mamlaka yaliyo kwenye Agano la Kale, na ahadi zimeandikwa humo. Na kila wakati ninazishika na kuzitendea kazi, na kunipa ujasiri, na kwamba muunganiko wa imani unanipa mambo ya maisha **kama vile kile kilichomfufua Kristo katika wafu**. Na mambo ya maisha mapya yanaweza kubadilisha asili yangu kama malighafi za mionzi ya radio, isiyoonekana, inaweza kubadilisha muundo wa chembe chembe za seli kama ukizishika.

Mungu anaweka maisha ndani yetu yanayoweza kuzaliana, ndiyo maana ukiroho ni udhihirisho war roho, ndiyo maana haki inaitwa tunda la roho. Ni maisha mapya yanayokuwa kupitia sisi na yanaweza tu kuendelea kwa imani katika neno, lakini yalianzishwa na kuimarishwa kupitia mwamba imara uliojaribiwa na kuthibitishwa "Alifufuka katika wafu," na hii inanipa mimi imani ya kuamini kwamba atatenda jambo lingine kama alivyosema, ambalo ni kurudi tena.